Office of
Immigrant Affairs
CITY OF PHILADELPHIA

# Taarifa kuhusu COVID-19 kwa wahamaji, wakimbizi na watafuta hifadhi

**Ukurasa huu utasasishwa na maelezo mapya kadri yanavyopatikana. Angalia mara kwa mara.**

Ifuatayo ni orodha ya taarifa kwa wahamaji, wakimbizi, watafuta hifadhi na mashirika yanayohudumia jamii hizi huko Philadelphia. Ilisasishwa mwisho tarehe 23 Aprili, 2020.

Kwa kuwa maelezo yanabadilika kwa haraka, unapaswa kupiga simu kwa nambari 1-800-722-7112 ili kuwasiliana na mtaalam wa matibabu, piga 3-1-1 ikiwa una maswali kuhusu huduma za Jiji au tembelea tovuti ya www.phila.gov/covid-19 kwa taarifa zinazochipuka.

Kwa wakati huu ambao hakuna uhakika wa hali halisi, hakikisha maelezo yote yanayohusiana na COVID-19 yana asili ya kuaminika.

---

## Maelezo ya Jumla

### Ufikiaji wa Lugha

- Maelezo muhimu mara kwa mara hutafsiriwa kwa lugha ya Kihispania, Kichina Kilichorahisishwa, Kivietinamu, Kirusi na Kifaransa.
- **Angalia hapa** ili upate maelezo yaliyochaguliwa katika lugha zingine ikijumuisha Kiarabu, Lugha asili ya Kihaiti, Kiswahili, Lugha ya Khmer, Kiindonesia na Kikorea.
- Huenda maelezo kutoka kwa mashirika ya kijamii yatatafsiriwa au yakose kutafsiriwa katika lugha za ziada.

# Kuendelea kuwa na Ufahamu wa Yanayojiri

## Taarifa za Jiji

- Kwa maelezo ya jumla, tembelea tovuti ya www.phila.gov/covid-19. Taarifa zilizotafsiriwa zinapatikana.
- Kwa taarifa za kila siku kuhusu jinsi Jiji linavyokabili COVID-19, tazama maelezo mafupi kutoka Jumatatu hadi Ijumaa kuanzia saa 1:00 p.m. Taarifa za moja kwa moja za umma zinapatikana mtandaoni katika:
  - Akaunti ya Twitter ya Idara ya Afya ya Umma (@PHLPublicHealth) pamoja na akaunti za Facebook.
  - Phila.gov/PHLgovTV.
  - Idhaa 64 na 1164 za Comcast.
  - Idhaa 40 na 41 za Verizon.
- Ili kupata arifa kwa simu yako, tuma COVIDPHL kwa 888-777.
- Kwa maswali yanayohusiana na afya, pigia 1-800-722-7112.
- Kwa maswali yanayohusiana na huduma za Jiji, pigia 311. Ufasiri unapatikana, tafadhali subiri operata ili uwasilishe ombi la lugha yako.

## Sasisho za Wilaya ya Shule za Philadelphia

- Angalia tovuti ya Wilaya ya Shule za Philadelphia ili kupata sasisho. Taarifa katika lugha nyingi zinapatikana.
- Shule zitabakia zimefungwa katika mwaka wote wa shule, lakini mafunzo yataendelea. Wanafunzi wanaweza kuazima Vipatakilishi vya Chromebook kwa mafunzo ya mbali.
- Wanafunzi wanaweza pia kupata vyakula bila malipo na miongozo ya mafunzo.
- Familia ambazo zina maswali ya jumla au zinahitaji msaada kuhusu miongozo ya mafunzo zinaweza kupigia Wilaya ya Shule za Philadelphia kupitia 215-400-5300. Usaidizi unapatikana katika lugha zingine. Nambari za mawasiliano za Wilaya zinafanya kazi kuanzia saa 9:30 am - 2:30 pm.

## Sasisho za SEPTA.

**Huduma ya SEPTA:** SEPTA inalenga kuongeza viwango vya huduma, **na ratiba za kawaida za mabasi yote, Reli za chini ya ardhi na troli** zikirejea katika wiki ya tarehe 17 Mei. Meneja Mkuu wa SEPTA Leslie S. Richards alisema "SEPTA inatambua kuwa waendeshaji wetu

watatutazamia katika wiki zijazo kwani vizuizi vinatarajiwa kulegezwa. Bado tunahimiza kusitishwa kwa safari zisizo za lazima na tunaiona hii kama fursa ya kupunguza msongamano na kutekeleza hali ya kutokaribiana kwenye magari yetu. Tungependa kuwakumbusha waendeshaji kwamba kutokuwepo kwa watu bado ni changamoto kubwa, na kwamba wanapaswa kuwa tayari kwa kukatizwa kwa huduma katika wiki zijazo. "

### Sasisho za Uchaguzi

Kufuatia janga la COVID-19, uchaguzi wa kimsingi wa urais 2020 katika jimbo la Pennsylvania umeahirishwa hadi tarehe 2 Juni, 2020. Ili kujifunza zaidi kuhusu jinsi ya kujisajili kupiga kura na jinsi ya kutuma ombi la kupiga kura kwa njia ya barua, angalia blogu hii.

- Tarehe 18 Mei ndio tarehe mpya ya mwisho ya kujisajili kupiga kura Pennsylvania.
- Tarehe 26 Mei ndio siku ya mwisho ya ofisi yako ya kaunti kupokea maombi ya upigaji kura kwa njia ya barua.
- Tarehe 2 Juni ndio siku ya uchaguzi wa kimsingi wa rais Pennsylvania. Upigaji kura utafunguliwa kuanzia 7 a.m. hadi 8 p.m. Mradi tu uwe kwenye laini itimiapo saa 8 p.m., utaweza kupiga kura. Kura zilizopigwa kwa njia ya barua ni lazima pia zirudishwe itimiapo saa 8 p.m. siku ya uchaguzi.

Kwa maelezo zaidi kuhusu upigaji kura na maeneo ya kupiga kura, tembelea philadelphiavotes.com.

---

# Jinsi ya Kudumisha Usalama

## Amri ya Kukaa Nyumbani

Amri ya Kukaa Nyumbani na Shughuli ya Kibiashara la Jiji la Philadelphia inahitaji wakazi wa Philadelphia (ambao hawatoi **huduma muhimu na za lazima** au kuendesha shughuli za haraka za kimaisha) kukaa nyumbani. Njia bora zaidi ya kuzuia kuenea kwa Virusi vya Corona vya COVID-19 ni kuwazuia watu ambao wameambukizwa kutotangamana na wale ambao hawajaambukizwa. Hii inamaanisha kuwa kila mtu anapaswa kuzingatia hali ya kutokaribiana na wengine na biashara zisizo za lazima zifungwe. Angalia hapa ili kupata orodha ya bishara muhimu na za lazima na zile zisizo za lazima.

## Fuata Miongozo ya Afya ya Umma

- Nawa mikono yako, weka futi sita kati yako na mwenzako ili kuzingatia hali ya kutokaribiana, vaa vibarakoa ili kujikinga na kuwakinga wengine, na ukae nyumbani wakati wote inapowezekana. Maelezo zaidi yako hapa.
- Kuvaa barakoa katika maeneo yenye watu wengi. Ni moja ya njia bora zaidi za kujilinda na kuwalinda wengine. Soma vidokezo hivi kuhusu jinsi ya kuvaa barakoa yako.
- Jikumbushe kupitia Vidokezo vya Mazungumzo ya Kiongozi wa Jamii na Mabango Yanayoashiria Hali ya Kutokaribianayaliyowekwa na Idara ya Afya.
- Kuwa Kapteni wa Mipangilio ya Jamii ya Kukabiliana na COVID-19. **Jisajili** ili kupata mafunzo pamoja na timu ya Philly Counts. Vipindi vinapatikana katika lugha ya Kiingereza, Kihispania, Kichina na Kifaransa.
- Vituo vya Kudhibiti Magonjwa vina taarifa nyingi katika lugha tofauti ambazo zimetafsiriwa na majiji mengine hata katika lugha zaidi kama Kikorea, Kikaren, Kitigrinya, Kiamhariki, Kiburma na Kinepali.

## Pimwa

**Pata kituo cha upimaji karibu nawe:** Mfumo mpya wa kupata kituo cha upimaji kwenye **phila.gov/testing** unawasaidia watu kupata upimaji wa COVID-19 bila malipo hapa Philadelphia. Mtu yeyote anaweza kutafuta kituo kwa kutumia anwani, kubofya eneo la ramani ili kupata habari maalum ya kituo na kuchuja kupitia siku ya wiki na njia ya kuendesha gari au ya kutembea.

- Kila kituo cha upimaji kina mahitaji yake na maelezo hayo yamejumuishwa katika kila eneo kwenye ramani. Kwa mfano, vituo vingine vinahitaji rufaa, miadi, au vigezo fulani vya kufuatwa na wagonjwa. Hakuna vituo vinavyohitaji malipo, bima au dhibitisho la uraia. Wakazi wanahimizwa sana kupiga simu kwanza ili kupata miadi au rufaa; nambari zote muhimu za simu zinapatikana kwenye ramani.
- Mfumo wa kupata vituo unapatikana katika lugha sita na ramani itaendelea kusasishwa jinsi vituo vipya vya upimaji vinavyozidi kufunguliwa.
- Upimaji zaidi unapatikana Philadelphia. Soma miongozo ya upimaji wa COVID-19. Angalia mara kwa mara kwani miongozo itabadilika kulingana na upatikanaji wa upimaji.

**Viwango Vya Upimaji Vilivyopanuliwa:** Idara ya Afya ya Umma ya Philadelphia sasa inapendekeza upimaji wa virusi vya korona vya COVID-19 kwa mtu yeyote bila kujali umri,

ambaye ana kohoa upya, anakabiliwa na upungufu wa kupumua, au mbili ya dalili zifuatazo: homa ya joto, baridi, maumivu ya misuli, koo kavu, maumivu ya kichwa, upotezaji mpya wa ladha au harufu. Upanuzi wa mapendekezo ya upimaji unafuatia kuongezeka kwa upatikanaji wa upimaji wa virusi vya korona katika maabara ya afya ya umma na ya kibiashara. Kuongeza upimaji wa virusi vya korona ni sehemu muhimu ya mpango wa Jiji na wa Pennsylvania wa kufungua tena kwa njia salama.

> Unaweza kupokea huduma ya matibabu isipojalisha hali yako ya uraia na uwezo wako wa kuzungumza katika lugha ya Kiingereza. Soma kuhusu sera za Philadelphia kuhusu makaribisho na haki zako katika mipangilio ya matibabu.

---

# Mahali pa Kupata Msaada

## Usaidizi wa Dharura wa Fedha

Wafiladelfia ambao wanatatizika kifedha kwa sababu ya janga hilo wanaweza kustahiki kupata fedha za dharura kutoka Idara ya Huduma za Binadamu ya Pennsylvania. Programu ya Usaidizi wa Dharura ni ya familia zilizo na watoto na ambazo zilikuwa na waliokuwa wakifanya kazi na wakapoteza mapato au ajira. Familia ambazo mapato yao yapo chini ya asilimia 150 ya kiwango cha umaskini cha serikali - takriban $ 2,700 kwa mwezi kwa familia ya watu watatu - wanastahiki. Familia zinazostahiki zitaweza kupata ruzuku ya wakati mmoja ya takriban $ 400-$ 1,200, kulingana na ukubwa wa familia zao.

## **Sasisho za Sheria ya Shirikisho kuhusu CARES**

- Sheria ya CARES ni kifurushi cha usaidizi iliyopitishwa na serikali ya shirikisho ili kutoa msaada katika janga la COVID-19. Chunguza ili ujue kiwango cha pesa za msaada unazoweza kupata na kile unachohitaji ili kupata pesa hizo..
- Ikiwa unahitaji usaidizi katika kulipa ushuru au kufungua akaunti ya benki, pigia Mshauri wa Uwezeshaji wa Kifedha kupitia 1-855-FIN-PHIL.
- Angalia Huduma za Kisheria za Umma ili kupata maelezo zaidi kuhusu Sheria ya CARES—haswa ikiwa unapokea faida za SSI au SSDI na una watoto walio chini ya umri wa miaka 17. Unaweza kupokea $ 500 ya ziada kwa watoto wako lakini lazima uwasilishe fomu ya ziada ya ulipaji ushuru.

# Msaada wa Kisheria kuhusu Uhamaji

- Ofisi za USCIS zimefungwa lakini maombi yaliyotumwa bado yanashughulikiwa. Angalia USCIS kwa maelezo zaidi.
- Kituo cha Hudumua Zinazohusinana na Uraia, HIAS-PA, na mashirika ya kijamii kama vile Juntos yako hapo kusaidia pia.

## Msaada wa Chakula

Jiji limeanzisha mfumo wa kupata chakula (http://phila.gov/food) ambao unatoa maelezo katika lugha sita na unajumuisha programu ya chakula inayosaidiwa na Jiji, vyakula vya wanafunzi, vyakula vya wazee na maeneo ya nje.

Pia kunazo taarifa bila malipo kuhusu ujauzito, unyonyeshaji, msaada kwa watoto zinazopatikana wakati huu wa COVID-19.

## Msaada wa Makazi na Huduma za Kawaida

- Huduma za intaneti na simu ya mkononi kwa bei nafuu.
- Ufukuzaji na uchukuaji wa nyumba za mkopo zimesitishwa kwa muda.
- Maji, gesi, na stima kukatwa pia kumesitishwa.
- Tarehe ya mwisho ya ulipaji ushuru ya mali Philadelphia imesogezwa hadi tarehe **15 Juni.** Kwa maelezo kuhusu jinsi ya kulipa, tembelea sasisho ya Idara ya Ushuru.

# Manufaa ya Umma

- Kupokea utunzaji wa kimatibabu kwa ugonjwa wa COVID-19 hakuzingatiwi katika maamuzi ya malipo ya umma. Kwa maelezo zaidi, tembelea USCIS au pigia Huduma za Kisheria za Umma kupitia 215-981-3700.
- Manufaa ya ukosefu wa ajira hayahesabiki katika maamuzi ya malipo ya umma kulingana na USCIS. Angalia Ofisi ya Fidia ya Ukosefu wa Ajira ya Pennsylvania ili upate sasisho kwani manufaa yanaweza kupanuliwa. Wasiliana na Usaidizi wa Kisheria wa Philadelphia na Huduma za Kisheria za Jamii ikiwa una maswali mengine.

- Manufaa kwa waliokosa ajira hayazingatiwi katika maamuzi ya malipo ya umma kulingana na USCIS. Angalia Ofisi ya Pennsylvania ya Fidia ya Ukosefu wa Ajira ili

kupata taarifa kwa kuwa manufaa yanaweza kuongezwa. Wasiliana na Usaidizi wa Kisheria wa Philadelphia ikiwa una maswali ya ziada.

- BenePhilly anaweza kukusaidia kuwasilisha ombi ili upate manufaa tofauti. Piga simu kwa 844-848-4376.
- PCCY inaweza kukusaidia kupata bima ya matibabu kwa mtoto wako na kwako pia. Piga simu kwa 215-563-5848, ext. 17 ili kupata msaada katika lugha yako.
- Ustahiki wa kupokea Usaidizi wa Dharura wa Matibabu umepanuliwa ili kujumuisha COVID-19. Wasiliana na Huduma za Kisheria za Jamii ili kupata maelezo ya jinsi ya kutuma ombi.

## Haki Zako Kazini

- Kwa kuzingatia COVID-19, Philadelphia imeongeza Muda wa Mapumziko kwa Mfanyakazi aliye Mgonjwa, atakayelipwa hata katika muda huu. Wafanyakazi husika wanaweza kutumia muda wao wa mapumziko kaitika ugonjwa kwa maswala mengine yanayohusiana na COVID-19 na utunzaji wa kinga bila kuogopa kuadhibiwa.
- Sheria ya Kazi ya Haki katika Wiki ya Philadelphia inatekelezwa. Angalia ni sehemu gani za sheria zinatumika wakati wa janga.
- Kwa maelezo zaidi kuhusu haki zako ukiwa kazini, tembelea Huduma za Kisheria za Jamii kwenye Maswali Yanayoulizwa Sana.

## Msaada kwa Biashara Yako

- Sheria ya shirikisho kuhusu CARES inatoa usaidizi kwa biashara ndogo ndogo. Angalia maana ya hili katika biashara yako au tembelea Ushirikiano wa Kitaifa kwa Wamarekani Wapya ili upate muhtasari.
- Philly VIP inaweza kusaidia mashirika yasiyo ya faida na biashara ndogo ndogo kupata msaada wa kisheria bila malipo. Jisajili ili upate mashauri mtandaoni bila malipo.
- Idara ya Leseni na Ukaguzi imetoa mahitaji mapya ya miradi ya ujenzi chini ya COVID-19. Angalia hapa kwa maelezo zaidi.
- Idara ya Biashara imetoa miongozo ya jinsi ya kulinda biashara yako katika muda huu mfupi wa kufungwa kwa biashara.

## Msaada kwa Afya ya Kiakili, Ulevi na Ulemavu wa Kiakili

- Jiji la Philadelphia linatoa huduma za afya ya kiakili, ulevi na ulemavu wa kiakili.
- Kwa huduma ya afya ya kiakili na ulevi, piga simu kwa Afya kuhusu Tabia ya Jamii inayopatikana kila wakati kupitia 888-545-2600.
- Kwa shida kubwa za afya ya kiakili, piga simu kwa 215-685-6440 inayopatikana kila wakati.
- Ili kuwashughulikia wanaohitaji matibabu ya mara moja ya uraibu wa dawa za kulevya, wasiliana na NET Access Point kupitia 844-533-8200 au 215-408-4987.
- Kwa huduma za ulemavu wa kiakili, pigia Idara ya Huduma za Afya kuhusu Tabia na Ulemavu wa Kiakili kupitia 215-685-5900.
- Taarifa na maelezo yanapatikana ili kukuza matumizi ya dawa yaliyo salama wakati huu wa COVID-19.

## Msaada katika Dhuluma za Nyumbani

- Ulinzi kutokana na unyanyasaji na dhuluma za nyumbani unapatikana wakati huu wa COVID-19.
- Kuripoti Dhuluma au Kupuuzwa kwa Mtoto wakati huu wa COVID-19..
- Nambari ya Simu, 866-723-3014 iliyo ya Dhuluma za Kinyumbani huko Philadelphia imefunguliwa kila siku, kila wakati.
- Ikiwa unataka ulinzi wa kisheria, unaweza kutafuta msaada katika Sehemu ya Dharura kwenye Kituo cha Sheria ya Haki ya Uhalifu, Chumba B-03 1301 Filbert St., Philadelphia, PA 19107.
- Piga simu kwenye Kituo cha Sheria cha Wanawake Dhidi ya Dhuluma kupitia 215-686-7082 ukitumia nambari salama ili wakili aweze kuwasiliana nawe.
- Kituo cha Hudumua Zinazohusiana na Uraia kina nambari za simu za upangaji wa usalama na msaada wa kisheria katika lugha nyingi.
- Wanawake Waliojipanga Dhidi ya Ubakaji (WOAR) ina nambari ya simu, ambayo ni 215-985-3333, inayopatikana kila siku, kila wakati ili kusaidia waathirika wa tabia mbaya, dhuluma na unyanyasaji ya kijinsa. Piga simu kupitia 215-985-3315 kwa maelezo zaidi kuhusu huduma zinazotolewa na WOAR.

## Kuripoti Uhalifu wa Chuki na Matukio ya Upendeleo

- COVID-19 inatuathiri sisi sote. Uhalifu wa chuki wenye misingi ya kikabila na hofu ya maambukizi ya Virusi vya Corona ni kinyume cha sheria.

- Wasiliana na Tume ya Philadelphia Kuhusu Uhusiano wa Kibinadamu kupitia pchr@phila.gov au 215-686-4670 ili kuripoti matukio ya chuki au upendeleo.
- Taarifa za ziada kutoka kwa Tume ya Uhusiano wa Kibinadamu ya Pennsylvania kuhusu uhalifu wa chuki kote nchini.

---

# Taarifa za Jimbo Lote

- Kwenye tovuti ya Jimbo la Pennsylvania kuna maelezo zaidi kuhusu COVID-19. Angalia hapa pia, kwa mwongozo kuhusu manufaa ya kupiga kura na ukosefu wa ajira.
- Kwenye Muungano wa Raia wa Uhamaji wa Pennsylvania kuna mwongozo wa taarifa zinazohusiana na COVID-19 katika jimbo la Pennsylvania.